**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**HALMASHAURI YA MJI WA MBULU**

**SHULE YA SEKONDARI TUMATI**

**NAMBA ZA SIMU**

**Mkuu wa Shule … 0624051320**

**M/mkuu wa shule..... 0688368213**

**Mwl Malezi------0763006494/0763806494**

**Taaluma………0769931709/0784282250**


**Shule ya Sekondari… TUMATI**

**S.L.P 197, Mbulu Manyara**


**Tarehe………………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………...........................................................................**

**S.L.P ………………………………….................**

Yah**:** MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA **TANO** KATIKA SHULE YA SEKONDARI **TUMATI**, HALMASHAURI YA **MBULU (DC)**, MKOA WA **MANYARA,** MWAKA…………………

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………….. na atasoma tahasusi ya ……………………L.

Shule ya Sekondari **TUMATI** ipo umbali wa **Kilometa 7** Mashariki mwa Mji wa DONGOBESH Usafiri wa bodaboda/ bajaji kutoka mjini **Dongobesh** unapatikana katika kituo cha mabasi **Dongobesh** Nauli ni Shilingi **3,000 Bajaji** na Shilingi **3000** kwa Bodaboda.

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………………………………** Mwisho wa kuripoti ni tarehe……………………………

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

i) Sare ya shule hii ni sharti nyeupe **pea mbili**. Mikono mirefu, sketi (2) rangi ya darkblue lenye rinda urefu chini ya magoti ,suruali (2) rangi ya darkblue na sweta rangi ya darkblue kwa wasichana .

ii) Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama atakayotumia darasani na hijab nyeusi ya kushindia

iii) Sare ya michezo ni T-shirt ya rangi ya blue, sketi rangi blue (mshono wa mwavuli), skin tight nyeusi na raba za michezo jozi moja Rangi nyeupe.

iv) .Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi vinavyo funika mguu.

v) Soksi jozi mbili nyeupe za shule.

vi) .Nguo za kushindia traki nyeusi moja, shamba dress – sketi nyeusi (kitambaa kizito mshono wa rinda boksi) na t-shirt rangi nyeupe yenye kola.

vii) .Ndala za kuogea.

viii) .Tai rangi ya darkblue yenye michirizi/mistari meupe.

ix) .T-shirt ya shule ataikuta shuleni kwa bei nafuu.

x) Pullneck mbili rangi nyeupe kwa ajili ya baridi.

**3. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 (counter book Q4), kalamu za kutosha, Rula, mathematical set, Scientific calculator (Non programmable calculator Casio Fx-991), **Ream Mbili (A4)** kwa mwaka na Dissecting kit na tray kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi CBG & CBA. (*Ream, madaftari (counterbook), scientific culculator na dissecting kit inapatikana shuleni kwa bei nafuu*).

ii. Barua ya maagizo (Joining instruction)

iii. **Vyeti vyako (Vivuli vya vyeti) vya kidato cha nne (IV) Academic, Leaving na cheti cha kuzaliwa**.

**iv. Cheti cha daktari (medical Examination Certificate) ambacho kimejazwa vizuri na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali**

**v. Fomu ya makubaliano ya mzazi kumsomesha mwanae (Fomu zimeambatanishwa nyuma ya barua hii)**

vi. Mto mmoja na foronya 2 za rangi ya blue bahari.

vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya PINK 1 & BLUE BAHARI 1, blanket 1 nzito, Taulo (1) na nightdress

viii. Mwavuli 1, na tochi pamoja betri zake.

ix. Aje na Godoro 1 size $2^{1/2}$x3x6.

x. Vyombo vya chakula: - Sahani ya bati, (Aluminium) kikombe, bakuli na kijiko( ***vinapatikana shuleni kwa bei nafuu***)

xi. Sanduku la bati/chuma la kufunga kwa kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyako.

xii. Mwanafunzi aje na BIMA ya Afya kwa ajili ya matibabu yake. (*kwa wale ambao wanayo bima*)

xiii. NB: Gharama nyingine ya dawa nje ya bima atagharimia mzazi, shuleni tunatoa huduma ya kwanza tu.

xiv. Ndoo tatu (3) yenye ujazo wa lita 10 zenye mifuniko, mbili kwa matumizi yake binafsi na moja kwa ajili ya shughuli za usafi shuleni

xv. Jembe 1 lenye mpini imara kwa ajili ya kazi za shule.

xvi. Mopa 1,kwanja/fyekeo 1,ufagio wa chelewa 1,soft broom 1, hard broom 1, sabuni ya maji 2.5Ltrs kwa ajili ya kufanyia usafi.

xvii. Nguo za ndani za kutosha

xviii. Mwanafunzi kwa TAHASUSI yake anashauriwa kujinunulia vitabu vya ziada na kiada kama ifuatavyo;

(a) Somo la Biolojia anunue vitabu vifuatavyo;

(i) ***Biology for advanced level sec school student's book*** form five BY T.I.E

(ii) ***Biology for advanced level secondary school students's book*** form six by T.I.E

(iii) ***Biological Science*** 1&2 3rd edition by D.J Taylor.

(iv) ***New understanding biology*** 4th edition by Glenn.

(b) Somo la Agriculture anunue vitabu vifuatavyo;

(i) ***Agriculture for advanced secondary school student's book***; form five by T.I.E

(c) Somo la Kemia anunue vitabu vifuatavyo;

(i) General and inorganic chemistry by T.I.E

(ii) organic chemistry for advanced level by T.I.E

(iii) Physical chemistry by T.I.E

(iv) Conceptual chemistry class xi volume1, by Chandy S.

(v) conceptual chemistry class xii by Chandy S.

(vii) Alevel chemistry 4th edition by Ramsden E.N.

(d) Somo la Jiographia anunue vitabu vifuatavyo;

(i) Pracrical Geography by TIE

(ii) Physical Geography by TIE.

(e) Somo la history anunue vitabu vifuatavyo;

i. .History for advanced level sec school student's book form five BY T.I.E

ii. History for advanced level secondary school students's book form six BY T.I.E

(f) Somo la english language

i. English for A-LEVEL FORM FIVE TIE

ii. English for A-LEVEL FORM SIX TIE

iii. Competence in Linguistics, English language form five. Mgonja M,E

**PLAYS.**

-*An Enemy Of The People*

*-The Government Inspector*

*-A Taste Of Heaven*

**NOVELS.**

**-**Animal Farm

*-Chasing The Leopard Finding The Lion*

*-The Orppotunist Elite*

*-The Horrizon Unvelled*

**POETRY.**

*Summons. Poems From Tanzania*

*Poets of africa,lament of the silent&other poems*

xix. Koti la maabara-rangi nyeupe (laboratory white coat) kwa ajili ya kuvaa wakati wa mafunzo kwa vitendo akiwa maabara kwa wanafunzi masomo ya sayansi.

xx. Rain boot pair 1 (**rangi nyeupe**), ya kuvaa maabara na shambani wakati wa mafunzo kwa vitendo.

xxi. Pazia pair moja (rangi ya light blue) kwa ajili ya kuweka madirishani.

**4. Michango mbalimbali**

| ***S/N*** | ***MICHANGO*** | ***KIASI*** |
|---|---|---|
| **1.** | **Uendeshaji wa shule. 65,000/= Kitambulisho. 5,000/=. Tahadhari. 5,000=. Nembo ya Shule 5,000/=** | **Jumla ni 80,000/= (KWA MWAKA)** |
| **2.** | **Bima ya Afya ni Shilingi 50,400 tu italipwa na wale wanafunzi wasio na bima za Afya.** | |
| | | |

***N:B*** Fedha zote zilipwe Benki ya NMB kwa **Ac.No** 41201200078 kwa jina la **TUMATI SECONDARY SCHOOL-RECCURENT** isipokuwa fedha ya bima ya afya(TSH 50,400) ziletwe shuleni**.** Wenye kadi ya Bima ya Afya waje nazo shuleni.

Utakapofika shuleni unatakiwa kuwasilisha **"bank pay-in slip**" kwa mhasibu wa shule ili akuandikie stakabadhi ya malipo.

## 5.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**6. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamojana:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wotewawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**7. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule……………………………..**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**Mkuu wa shule …0624051320**

**M/mkuu wa shule..0688368213**

**Taaluma...0769931709/0784282250**

**Malezi....0763006494/0763806494**

**Matron....0758141507**

**Patron 0763006494/0763806494**

**FOMU YA TAARIFA MAALUM KUHUSU MWANAFUNZI**

**(Taarifa zote zijazwe kwa herufi kubwa)**

**SEHEMU A:**

Jina kamili …………………………….. Tarehe ya kuzaliwa ………………

Kabila ………………... Dini ………………........

Jina la Mzazi/Mlezi ……………………. Anwani ya Nyumba................................

Kijiji ……………………. Kata ……………………… Tarafa……………………...

Wilaya ……………………. Mkoa …………………………..

**SEHEMU B:**
Kazi ya wazazi/Mlezi ………………………………………………………
Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………..
**SEHEMU C:**
Mambo ambayo unapendelea kufanya baada ya muda wa masomo (kama Michezo,Bustani).
**(1)………………......(2) …………………..**

**SEHEMU D:**

**Ndugu na jamaa (Kufuata umri wao) ambao wataruhusiwa kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni.**

| **Majina ya Ndugu Na picha (passport size)** | **Umri** | **UHUSIANO** | **Kiwango cha Elimu** | **Anwani** | **Simu** |
|---|---|---|---|---|---|
| BABA | | | | | |
| MAMA | | | | | |
| NDUGU 01: | | | | | |
| NDUGU 02: | | | | | |

**Naahidi kuwa na tabia nzuri mchapakazi na mwenye bidii katika masomo.**

**Sahihi ya Mwanafunzi………………………………………………..**

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi …………....... Tarehe ......……………...**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHULE YA SEKONDARI TUMATI**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE.**

**Fomu hii irudishwe Shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi ikiwa imejazwa kikamilifu.**

**A: MWANAFUNZI**

Mimi ......................................................................... nimesoma kwa makini maagizo

ya kujiunga na shule hii, Pia sheria za Shule. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/nimeikataa nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu:-

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

Tarehe ……………………………………. Sahihi …………………………………

**B. MZAZI / MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUMSOMESHA MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………… wa kijiji cha …………………… ….

Kata ya ………………………………Halmashauri ya……………………………

Ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………...……………..

Anayeingia kidato cha …………………………….. katika shule ya sekondari TUMATI najifungia wajibu huu kwa ajili ya kumsomesha mwanafunzi tajwa hapo juu mbele ya utawala wa kijiji changu hiki. Nimesoma barua ya kumwita shuleni, sheria za shule na fomu zote zilizoambatishwa, nimeelewa kila kitu na kuridhika. Pia najua nisipotimiza masharti yote mwanafunzi huyu hatopokelewa shuleni. Nakubali ahadi hiyo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kuikiuka bila hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.

Sahihi ya mzazi au mlezi ……………………………..Tarehe ………………..

Sahihi na mhuri ya afisa mtendaji …………….Tarehe …………

Namba ya simu (afisa mtendaji)………...................

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM) AMBAYO ITAJAZWA NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Wilaya) ……………………………………………………………………… Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)………………………………………………….. Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

## A. HALI YA MWILI:

(i) Mapigo ya moyo ……………………………………………………………

(ii) Haemoglobin (HB) ……………………………………………………….

(iii) Kundi la damu (blood group) …………………………………………….

(iv) Mkojo (Urine) …………………………………………………………..

(v) Kinyesi (stool) …………………………………………………………..

(vi) Macho (Eye) ……………………………………………………………

(vii) Masikio (Ear)…………………………………………………………….

Angalia:- Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i) – (vii)

## B. MAGONJWA:

*Amewahi/hajawahi/ana/hana/magonjwa yafuatayo:-

(a) Pumu …………………………………………………………………………

(b) Kifua kikuu ……………………………………………………………………..

(c) Kifafa …………………………………………………………………………

(d) Shinikizo la damu chini/juu ……………………………………………………..

(e) Vidonda vya tumbo …………………………………………………………

(f) Maradhi ya zinaa …………………………………………………………………….

(g) Ukoma ………………………………………………………………………………….

(h) Mental illness (ugonjwa wa akili ) …………………………………………………

(i) Maradhi mengine yasiyotajwa hapo juu:-

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

Sahihi na mhuri wa daktari /mganga

Tarehe ……………………………

**<u>RANGI NA MUUNDO WA USHONAJI SARE YA SHULE</u>**

| | |
|---|---|
| WASICHANA: RANGI YA DARKBLUE (SKETI NA SURUALI YAKE) |  |

| | |
|---|---|
| SURUALI RANGI DARKBLUE |  |
| SWETA RANGI YA DARKBLUE |  |

RANGI YA KITAMBAA NI DARKBLUE NAMBA MOJA